



SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 1
SOUAHELI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1
SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1

Thursday 17 May 2001 (afternoon)

Jeudi 17 mai 2001 (après-midi)

Jueves 17 de mayo de 2001 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Rédiger un commentaire sur un seul des passages.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento.

Kifafanue kimojawapo vya vifungu vifwataavyo:

1. (a)

5 Nchi hazikuhesabu ubora wa watoto wake, mpaka watoto wale walipokuwa wamepita maisha ya mwili; roho zao zilipokuwa zimevuka ng'ambo ya pili ambako upeo wa macho haukuweza kufika wala mwito wa mwanadamu haukuweza kusikilika, tena baada ya miili yao ilipokuwa imekwisha changanyika na vumbi la ardhi, na thamani yao yote kama viumbe bora ilipokuwa imepotea.

10 Kwa manzili kama haya mashtaka makubwa ya kupata habari zao yametokea mara kwa mara, kwa sababu alama imara ya nyayo zao zilikuwa zimekwisha futika mahala walipokanyaga, matendo yao mema yalikuwa yamezibwa na giza, maneno yao ya maana na mvuto yalikuwa yametoweka masikioni mwa watu wazima ambao fikira zao zilikuwa zimetatizika.

15 Rai ya kuzuia hasara kubwa kama hii haijapatikana bado, kwa sababu dunia imezowea sana kuwa pofu ya kuona bidii na matendo mazuri ya watoto wake katika wakati wa maisha yao ya mwili. Katika giza la sahu kuu ndipo ilipozinduka katika usingizi wake mzito, ikajaribu kuokota na kuunga pamoja viungo vya mkufu wa maisha bora, yaliyofumka kwa mapigo makali na mazito yaliyoangukia watoto wake walipokuwa wakijipambanua.

20 Mingoni mwa majina mashuhuri ya watu wa Afrika Mashariki pamotokea jila la mwanamke mmoja. Mwanamke mwenyewe aliitwa Siti binti Saad. Siti alikuwa binti wa wazazi Waafrika wa makabila mawili mbalimbali. Kuumeni alikuwa Mnyamwezi na kuukeni alikuwa Mzigua. Wazazi wake wote wawili walikuwa wazaliwa wa kisiwa cha Unguja.

Alikuwa mwanamke wa majina mawili katika nyakati mbalimbali. Kwa muda wa mika thelathini na moja ya kwanza alijulikana kwa jina la Mtumwa binti Saad, na katika miaka thelathini na tisa mingine alikwenda kwa jina la Siti binti Saad.

25 Mwanamke huyu alizaliwa Fumba na wazazi waliokuwa maskini. Baba yake alikuwa mkulima na mama yake alikuwa mfanyanji. Katika uzazi wake alifuatwa na ndugu wanaume wawili, Musa na Mbaruku; na umbu mmoja aliyeitwa Masika. Fumba kilikuwa kijiji kimoja katika vijiji vya Kisiwa cha Unguja. Kadiri ya umbali wa maili kumi na nne ulikuwa kati ya Mji wa Unguja na Fumba.

30 Tarehe, siku na wakati hasa wa uzazi wake vilikuwa vitu visivyojulikana. Wazazi wake waliokuwa maskini na wajinga wa kusoma hawakushughulika kuweka shajara la vitu vidogo kama wakati, siku au tarehe ya uzazi wa mtoto wao. Walakini, kwa kukisia ilidhaniwa kwamba tukio la uzazi wake lilitokea katika mwaka wa 1278 A.H au 1880 A.D, katika wakati, siku na tarehe ambayo haikujulikana.

Shaaban Robert, *Wasifu wa Siti Binti Saad*, 1970

1. (b)

Zamani Zimegeuka

	Zamani zimegeuka	geuko lenye hilaki
	Vilivyo juu hushuka	vya chini papo hubaki
	Mwenye chake huepuka	kana kwamba hakitaki
	Tuna mwendo wa samaki	haki hushindwa ni nguvu
5	Haki hushindwa ni nguvu	iko wapi tena haki?
	Husalia uonevu	na batili kujinaki
	Twaishi ja wapumbavu	hatuna pa kushitaki
	Tuna mwendo wa samaki	haki hushindwa ni nguvu
10	Twasikia na kuona	hatwambi kwa kudhihaki
	Haki ilivyosongana	hadi mwisho imesaki
	Wenye nguvu wamepona	wafile wapenda haki
	Tuna mwendo wa samaki	haki hushindwa ni nguvu
15	Zamani zatuonyesha	wanguvu hutamalaki
	Maguvu yao yatosha	mara huvumbua laki
	Na wanyonge wa maisha	ni wale wapenda haki
	Tuna mwendo wa samaki	haki hushindwa ni nguvu
20	Kaditama nimefika	huko mbele hakwendeki
	Limeshuka la kushuka	balaa haisemekiki
	Zamani zimegeuka	nyanya hainyekinyeki
	Tuna mwendo wa samaki	haki hushindwa ni nguvu

Ali Salim Zakwany, *Diwani ya Jinamizi*, 1979